OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

# MAADHIMISHO YA MIAKA 10 YA UTEKELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO




**2012 - 2022**

"Serikali ya Kidijiti"

Maadhimisho ya Miaka 10



# Ujumbe Kutoka kwa Waziri

Miaka kumi (10) ni hatua kubwa kwa maisha ya Taasisi, kama ilivyo kwa mtu binafsi. Wizara inajivunia sana mafanikio ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kutokana na jitihada inazozifanya za kuratibu na kukuza matumizi ya Teknolojioa ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi wa Taasisi za Umma.

Katika kipindi cha miaka 10, Mamlaka imekuwa miongoni mwa Taasisi za kuigwa nchini kwa utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi na tija. Mamlaka imeonesha umahiri mkubwa katika kusimamia na kuratibu matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, pamoja na kutoa huduma za Serikali Mtandao kwa kupitia Mifumo ya TEHAMA inayolenga kuboresha utendaji kazi katika Taasisi za Umma na utoaji huduma kwa Wananchi

Aidha, katika Dunia ya Uchumi wa Kidijiti tuliyopo sasa, TEHAMA ni nyenzo muhimu na wezeshi ili kufikia Mapinduzi ya 4 ya Viwanda katika Zama hizi za Taarifa (Information Age). Kwa umuhimu huo, Serikali imewekeza na kuweka kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA chini ya uratibu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, uliosaidia kujenga Miundombinu na Mifumo Tumizi na ile ya Kisekta inayowezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Tangu tuamue kubuni sera, mipango na mikakati madhubuti ya kutumia TEHAMA katika Taasisi za Umma, naamini sote tumeona manufaa yake. Kwa hakika tumepiga hatua ya kuridhisha katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Tunatambua kuwa, mafanikio haya hayakutokana na dhamira ya dhati na bidii ya Mamlaka peke yake, bali pia yametokana na michango ya wadau mbalimbali, wakiwemo Taasisi za Umma, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Utafiti na Taaluma, Taasisi Binafsi na Wananchi kwa ujumla..

Kipekee nimshukuru **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa dhamira na jitihada zake za wazi katika kujenga Serikali ya kidigiti, kwa kuongeza ajenda ya Serikali Mtandao kama eneo la kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili. Hii inaonesha umuhimu wa TEHAMA katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kuongoza uchumi wa viwanda

Kwa niaba ya Serikali napenda kuishukuru Mamlaka na wadau wote kwa kazi nzuri na naahidi kuwa Serikali itaendelea kutoa msaada unaohitajika kadri iwezekanavyo katika kutimiza azma ya Serikali Mtandao katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Mhe. Jenista Joackim Mhagama (Mb)**

*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora*


ii

# Ujumbe Kutoka Kwa Katibu Mkuu



Utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao ni moja ya maeneo muhimu ya maboresho yaliyofanyika katika Utumishi wa Umma, ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa Umma na kufanya zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

Kwa hakika Wizara inaridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka kwa kuwa imeweza kufanya mageuzi ya TEHAMA na kuboresha utendaji kazi wa kila siku katika Taasisi za Umma. Hivyo, ni fahari kubwa kwa Wizara, kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kutimiza miaka 10 tangu ilipoanzishwa Mwaka 2012, wakati huo ikiwa Wakala ya Serikali Mtandao

Wizara inatambua mchango wa Mamlaka katika utekelezaji wa jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendeleza jitihada za Serikali Mtandao hapa nchini. Mamlaka imefanikiwa kuweka mazingira wezeshi yaliyozisaidia Taasisi za Umma kutumia TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Mafanikio yaliyopatikana katika matumizi ya TEHAMA Serikalini yanatokana na jitihada na utashi wa pamoja wa Viongozi, Watendaji, Wananchi na Wadau wengine. Kwa upande wa Serikali tumeweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na kimkakati ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi ya TEHAMA yaliyo sahihi na salama, yenye ufanisi na tija katika kuwahudumia Wananchi na kuwaondolea kero mbalimbali

Wizara inatambua kuwa, mafanikio haya ya Mamlaka yamechangiwa na uadilifu, ubunifu, kuthamini wateja, kufanya kazi kwa bidii, ushirikiano na weledi katika utoaji wa huduma kwa Taasisi za Umma. Ni wazi kuwa, misingi hii imesaidia Mamlaka kuendelea kuwa Taasisi imara na inayoaminika.

Tunapoadhimisha historia ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Wizara inaendeela kusisitiza dhamira yetu ya kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma mtandao kwa Taasisi zote za Umma. Pamoja na hayo, tunaunga mkono juhudi za Serikali za kuleta mageuzi ya kidijiti yanayowezesha kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma.

**Dkt. Laurean Ndumbaro**

*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora*



# Ujumbe Kutoka Kwa Mwenyekiti wa Bodi

Katika kipindi cha miaka 10, Mamlaka ilijiwekea malengo kabambe na mahsusi ambayo mafanikio yake si tu yameboresha utoaji huduma kwa umma, pia yameongeza uwazi, pamoja na kupunguza gharama za utendaji kazi katika kuhudumia umma. Mafanikio haya pia yamewezeshwa na ubunifu, utengenezaji na usimamizi wa uendeshaji wa Mifumo na miundombinu ya Serikali Mtandao

Pamoja na dhamira ya kuboresha utoaji wa huduma, utekelezaji wa Serikali Mtandao unakusudia kufikia malengo ya kuimarisha utawala bora na kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa Taasisi za Umma, kwa kuhakikisha uwepo wa mawasiliano ya haraka, yenye uhakika na salama ndani na nje ya Taasisi za Umma, kuanzia kwenye Wizara, Mikoa hadi ngazi za Wilaya na Halmashauri, pamoja na Balozi zetu nje ya nchi.

Serikali Mtandao inadhamiria kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali, kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa muhimu katika kila ngazi Serikalini, kuimarisha usalama wa Serikali na raia wake katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia kwa kuongeza uwezo wa Serikali kupambana na majanga kwa kutumia teknolojia, kurahisisha michakato ya utendaji kazi katika Taasisi za Serikali na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Maendeleo ya matumizi ya TEHAMA ni muhimu kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi katika nchi yetu. Kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA kumefungua fursa mpya kwa Taasisi za Umma kufikia malengo yao kwa kutumia Serikali Mtandao.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, napenda kutoa shukrani za dhati kwa juhudi za makusudi zilizochukuliwa na Serikali za kutuunga mkono kwa kuandaa Sheria ya Serikali Mtandao iliyopitishwa na Bunge mwaka 2019 na Kanuni zake za mwaka 2020.

Sheria hii, pamoja na kuelekeza muktadha mzima wa utekelezaji wa Serikali Mtandao, imeweka msingi wa kisheria wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016 na kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kuipa jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendeleza utekelezaji wa Serikali Mtandao, pamoja na kusimamia uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma.

Matunda ya Sheria hii na Kanuni zake tumeanza kuyaona sasa kwa kuanza kuwa na matumizi ya TEHAMA sahihi na salama na yaliyooanishwa katika Taasisi za Umma, kwa Mifumo kuanza kuwasiliana na kubadilishana taarifa, hivyo kurahisisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

**Dkt. Mussa Kissaka**
*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi e-GA*

# Ujumbe Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu



Awali ya yote, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa juhudi za makusudi inazozichukua katika kujengea Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) uwezo wa kutekeleza majukumu yake ipasavyo hasa ikizingatiwa kuwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni nyenzo muhimu na wezeshi katika kuchochea ukuaji wa Mapinduzi ya 4 ya Viwanda na ujenzi wa uchumi wa kidijiti.

Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao, imewekeza katika kukuza na kuratibu matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma ikiwa ni pamoja na; kusimamia, kuendesha na kuendeleza mtandao wa mawasiliano Serikalinia, kujenga na kusimamia uendeshaji wa Mifumo shirikishi ya kimkakati na ya kisekta, kukagua, kupitia na kutathmini hali ya Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini pamoja na kutambua na kudhibiti matishio ya kiusalama mtandaoni. Lengo kuu la jitihada hizi ni kuboresha utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma kwa umma.

Ili kufanikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA Serikalini, uratibu wa jitihada za Serikali Mtandao ulianza kupitia Idara ya usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambapo kutokea Idara hiyo, Mwaka 2012 Serikali iliianzisha iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao kupitia Sheria ya Wakala za Serikali Sura Na. 245 na baadae Mwaka 2019 Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ilitungwa na kupitishwa, ambayo iliunda Mamlaka ya Serikali Mtandao na kuipa jukumu la kuratibu, kukuza na kuendeleza jitihada za Serikali Mtandao na kuhimiza uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

Katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, Mamlaka imefanikiwa kutekeleza malengo mbalimbali kulingana na Mpango Mkakati wa kwanza (2012/2013 – 2016/2017) na wa pili (2016/2017 – 2020/2021), pamoja na kuanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa tatu uliopo sasa (2021/22 – 2025/26) kwa ufanisi mkubwa uliotokana na utashi wa viongozi wa juu wa Serikali katika kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao kupitia Misingi Mikuu sita (6) ya utendaji kazi ambayo ni weledi, ubunifu, ushirikiano, kuthamini wateja, uadilifu, na kufanya kazi kwa pamoja.

Kutokana na jitihada hizi za Serikali, Mamlaka imewezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali ya utekelezaji wa Serikali Mtandao, kama vile uwepo wa Mifumo na Miundombinu shirikishi, ya kimkakati na ya kisekta ya TEHAMA, kuwezesha Mifumo ya TEHAMA kubadilishana taarifa, kuongezeka kwa huduma mtandao, kuongezeka kwa uwezo wa Taasisi za Umma kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao, kuongezeka kwa ubunifu katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao na kuimarika kwa uratibu na udhibiti wa jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na usalama wa taarifa za Serikali.

Pamoja na mafanikio yote yaliyopatikana, bado menejimenti na watumishi wa Mamlaka wana ari kubwa ya kuendeleza jitihada hizi kwa kiwango cha ufanisi mkubwa zaidi. Hii inatokana na ushirikiano mkubwa, pamoja na usimamizi na muongozo kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka. Hivyo basi, katika kuelekea miaka 10 ijayo, Mamlaka imeweka mikakati madhubuti itakayoongeza na kuimarisha zaidi mafanikio yaliyopatikana katika Serikali Mtandao.

Utekelezaji wa mikakati hii, pia utawezesha kuwa na sehemu moja ambapo huduma mtandao zote zitakuwa zinapatikana, kuongezeka kwa uwezo wa ubunifu kwa vijana wetu wa Kitanzania, kujenga uwezo wa kutengeneza vifaa na miundombinu ya TEHAMA (Hardware manufacturing), kujenga uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka ili kuwezesha utoaji wa huduma mtandao kwa wananchi hasa katika maeneo ya akili bandia, sarafu za kidijiti, pamoja na teknolojia za kifedha.

Aidha, kuimarika kwa serikali mtandao katika kipindi kijacho, pia kutapelekea kuongezeka kwa idadi ya Mifumo tumizi na ya kisekta ya TEHAMA inayobadilishana taarifa, kuongeza uwezo wa kudhibiti matishio ya usalama kimtandao, kuwa na namba moja ya utambuzi itakayowezesha utoaji wa huduma mtandao kwa urahisi, kutekeleza shughuli za utafiti na ubunifu ili kuongeza utoaji wa huduma kwa umma kupitia mtandao na kuwezesha matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka ili kurahisisha utekelezaji wa serikali mtandao,

Mwisho, na kwa kipekee napenda kuishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa jitihada zake za kuisimamia na kuiweka Serikali Mtandao kuwa eneo la kipaumbele katika kuboresha utendaji kazi katika Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa umma, pamoja na kuiwezesha Mamlaka kufikia malengo yake. Pia, naishukuru Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka kwa usimamizi na maelekezo sahihi, pamoja na kuwashukuru wadau mbalimbali kwa michango yao ya hali na mali katika kusaidia utekelezaji wa Serikali Mtandao, bila kusahau Menejimenti na watumishi wote wa Mamlaka, kwa juhudi kubwa na kujituma kwao kulikowezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa katika kipindi chote cha miaka 10.

**Mhandisi, Benedict Ndomba**
*Mkurugenzi Mkuu e-GA*

# Yaliyomo


**Ujumbe Kutoka kwa Waziri** ---------- ii

**Ujumbe Kutoka kwa Katibu Mkuu** ---------- iii

**Ujumbe Kutoka Kwa Mwenyekiti wa Bodi** ---------- iv

**Ujumbe Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu** ---------- v

**Historia ya Mamlaka ya Serikali Mtandao** ----------1

Dhana ya Serikali Mtandao ----------3

Miaka kumi ya Utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao ----------5

Uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake ----------6

Elimu Kwa Umma Kuhusu Utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao ----------8

Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao-----8

**Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini** ----------9

Mifumo ya Serikali Mtandao ---------- 11

Mifumo ya Kisekta ---------- 15

Miundombinu Shirikishi ya TEHAMA ---------- 19

Tafiti na bunifu za maendeleo ya Serikali Mtandao---------- 20

Mafunzo ya Serikali Mtandao ---------- 21

Ushirikiano na wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar ---------- 22

**Serikali Mtandao Miaka 10 ijayo---------- 23**

Mwelekeo---------- 24

Maeneo ya kipaumbele---------- 24

**Matukio Mbalimbali---------- 25**

**Michezo---------- 28**




# HISTORIA YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

# Historia ya Mamlaka ya Serikali Mtandao

## Kuhusu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

Mamlaka ya Serikali Mtandao ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, ikiwa na majukumu ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kusimamia uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za umma. e-GA ilianza kazi rasmi kutokana na Tangazo la Serikali **Na.964 la tarehe 6 Desemba, 2019,** lililoifuta iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao (eGA).

Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao Mwaka 2019 kunaendeleza afua za Wakala ya Serikali Mtandao iliyoundwa Aprili, 2012 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 Sura ya 245 ya mwaka 1997. Mamlaka, imerithi sehemu ya mipango ya iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao kwa sababu majukumu ya taasisi hizi yanafanana ingawa yametofautiana katika mamlaka ya utendaji.

Kabla ya kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao, matumizi ya TEHAMA Serikalini yalikuwa yanaratibiwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chini ya Idara ya Usimamizi wa Mifumo (DMIS) ambayo kwa sasa ni Idara ya Huduma za TEHAMA Serikalini (DICTS).

- **Dira**

Kutambuliwa kuwa Taasisi inayoongoza kwa ubunifu katika kuwezesha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma kwa umma.

- **Dhamira**

Kujenga mazingira wezeshi ya kisheria kwa ajili ya uratibu, usimamiaji na uendelezaji wa matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa umma.

- **Kaulimbiu**

“Uadilifu na ubunifu kwa utoaji wa huduma bora kwa umma”.

- **Misingi Mikuu**

Mamlaka inaongozwa na misingi mikuu sita (6) ambayo inaelekeza kuhusu tabia na mwenendo wa watumishi wake kwa ngazi zote. Misingi hiyo inafafanua utamaduni wa mahali pa kazi, kuhakikisha watumishi wote na wateja wa Mamlaka wana uelewa wa pamoja wa jinsi wanavyotakiwa kuhudumiwa na nini kinachotarajiwa kutoka kwao. Misingi hiyo ni:

(i) **Uadilifu:** Tunafuata viwango vya uendeshaji wa hali ya juu katika kila tunachofanya kwa kutambua kuwa, uhusiano wa kweli na uaminifu ni muhimu kwa mafanikio endelevu ya Taasisi.

(ii) **Ubunifu:** Tunazingatia utamaduni wa Mamlaka unaothamini uasili wa uvumbuzi na ubunifu katika kukuza vipaji kwa kuzingatia uwazi na ari.

(iii) **Kuthamini Wateja:** Tunajitoa kwa dhati kuwasaidia wateja wetu wa nje kutimiza malengo yao kwa kuelewa shughuli wanazofanya na kuwapa kile wanachokithamini zaidi.

(iv) **Kufanya kazi kwa Pamoja:** Tumedhamiria kufanya kazi kwa pamoja tukiwa na mawasiliano sahihi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

(v) **Ushirikiano:** Tunafanya kazi kwa uwazi na Taasisi za Umma na wadau wengine huku tukibadilishana taarifa, maarifa, uzoefu na tukitambua kuwa tunategemeana kwa maendeleo ya Serikali Mtandao.

(vi) **Weledi:** Tunazingatia ubora wa kazi kwa kiwango cha juu na kutoa huduma bora kwa wateja wetu.




# DHANA YA SERIKALI MTANDAO

# Dhana ya Serikali Mtandao


Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma. Lengo ni kutumia TEHAMA ili kusaidia kuongeza tija na ufanisi katika utendaji wa shughuli za Serikali na Taasisi za Umma (G2G), Serikali na Wananchi (G2C), Serikali na Watumishi (G2E), pamoja na Serikali na Wafanyabiashara (G2B) na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kwa kuzifanya huduma hizo zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.



# Miaka kumi ya Utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao

Katika kipindi cha miaka kumi (10), Mamlaka ya Serikali Mtandao imefanikiwa kutekeleza mambo mbalimbali ambayo yameleta mapinduzi katika matumizi ya TEHAMA, yakiwemo:

- Kujenga uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake.
- Kutoa elimu kwa umma kuhusu jitihada za serikali mtandao.
- Kusimamia uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao iliyoidhinishwa.
- Kuwezesha usanifu na ujenzi wa mifumo ya serikali mtandao ya kitaasisi na ya kisekta.
- Kuboresha na kusimamia uendeshaji wa miundombinu shirikishi ya serikali mtandao.
- Kusimamia na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya tafiti kwa ajili ya ubunifu katika serikali mtandao.
- Kusimamia utoaji wa mafunzo ya utekelezaji wa Serikali Mtandao.



# Uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake

Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), ilianza kazi Mwezi Julai, Mwaka 2012 baada ya kuteuliwa Mtendaji Mkuu na baadae watumishi wengine waliongezeka katika vipindi tofauti kulingana na uhitaji na ukuaji wa Taasisi.

Katika kipindi hiki cha miaka kumi (10), Serikali iliiwezesha Mamlaka kujizatiti katika maeneo mbalimbali yakiwemo: *Rasilimali watu, Mazingira ya Utendaji Kazi, Uboreshaji wa Mifumo ya Utendaji Kazi na Ustawi na Mafunzo kwa Watumishi.* Lengo la hatua hizi ni kuiwezesha Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

- **Rasilimali Watu**

Ili kuweza kutekeleza majukumu yake ambayo yamekuwa yakiongezeka kila Mwaka, Wakala ya Serikali Mtandao ambayo hivi sasa ni Mamlaka, imekuwa ikijiimarisha katika upande wa rasilimaliwatu katika kada mbalimbali kwa mujibu wa mahitaji kama yalivyoainishwa kwenye muundo wake wa utumishi

- **Mazingira ya Utendaji Kazi**
  - **Ofisi**

Mwaka 2012, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) ilipewa ofisi katika Jengo la UTUMISHI Dar es Salaam (ilipokuwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa majukumu yake. Kutokana na ukuaji wa Taasisi na ongezeko la watumishi, mwaka 2013 Ofisi za Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) zilihamishiwa katika jengo la TTCL-Extelecoms lililopo mtaa wa Samora Dar es salaam, baadae mwaka 2016, Wakala ya Serikali Mtandao ilifungua ofisi katika Mkoa wa Iringa. Aidha, mwaka 2017, Wakala iliitikia wito wa Serikali wa kuzitaka Taasisi zote za Umma kuhamia Dodoma kwa kufungua Makao Makuu ya ofisi ya muda katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mwaka 2019, kupitia mpango wa Serikali wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Serikali, Wakala ya Serikali Mtandao ikiwa ni moja ya Taasisi zilizojumuishwa katika mpango huo, mara baada ya kumaliza ujenzi wa jengo lake, ilihamia katika Ofisi zake zilizopo katika Mji wa Serikali Mtumba na mwezi Oktoba, 2021, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilifungua ofisi nyingine jijini Mwanza katika jengo la PSSSF.

- **Uboreshaji wa Mifumo ya Utendaji Kazi**

Katika kutekeleza matakwa ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali, Mamlaka iliunda kamati mbalimbali kwa lengo la kuboresha Mifumo yake ya utendaji kazi. Kamati hizo ni:- Kamati ya Ajira na Mafunzo, Kamati ya Maadili, Kamati ya UKIMWI na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY), Kamati ya Fedha na Bajeti, Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi (Risk Management Committee) pamoja na Kamati ya Zabuni.

- **Ustawi wa watumishi**

Mamlaka imeanzisha Mfuko wa Watumishi wa Kusaidiana (e-GA Social Fund-eGASF) pindi yanapotokea matukio ya dharura na yasiyotarajiwa kama vile misiba, maradhi, majanga n.k. Vilevile Mamlaka kupitia Kamati yake ya Ukimwi na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, imeendelea kusaidia watumishi wenye Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY).

- **Mafunzo kwa Watumishi**

Mamlaka imeendelea kutoa Mafunzo mbalimbali kwa watumishi wake yakiwamo yale ya muda mfupi na muda mrefu, pamoja na mafunzo maalumu yanayolenga kuboresha uwezo wa kiutendaji wa watumishi. Utekelezaji huu hufanyika kupitia mpango wa mafunzo wa mwaka ambao huandaliwa kutokana na mahitaji yaliyopo katika mwaka husika.

- **Ushirikishwaji wa Watumishi**

Mwaka 2015, Wakala ya Serikali Mtandao ilifanikiwa kuanzisha tawi la chama cha wafanyakazi (TUGHE) kwa lengo la kulinda maslahi ya watumishi mahala pa kazi, ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Tawi hili limekuwa ni jukwaa muhimu linalotumika kujadili mambo mbalimbali yanayohusiana na maswala ya kiutumishi, ikiwa ni pamoja na kushughulikia changamoto zinazowakabili watumishi kwa kuziwasilisha kwenye menejimenti na ngazi za juu za Chama cha Wafanyakazi pale inapobidi.



Washiriki wa Kikao kazi cha Mwaka cha Serikali Mtandao wakifuatilia Mada kwenye kikao hicho Januari 2019 katika Ukumbi wa Ndaki ya Sayansi ya Kompyuta Chuo Kikuu cha Dodoma.

- **Taarifa ya Fedha**

Kwa mujibu wa kifungu na 55 (1), cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao. Mamlaka huandaa na kutunza taarifa za fedha kutokana na shughuli zake kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya utoaji wa taarifa za fedha katika Sekta ya Umma (International Public Sector Accounting Standards).

Taarifa hizi za Fedha za kila Mwaka hukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Katika kipindi chote cha miaka kumi (10) Mamlaka imefanikiwa kupata Hati Safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

# Elimu Kwa Umma Kuhusu Utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao

Mamlaka imeendelea kuuhabarisha Umma kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa elimu kuhusu Serikali Mtandao kupitia vyombo vya habari, matangazo na mitandao ya kijamii.

Aidha, Mamlaka imefanya mikutano mbalimbali na Waandishi wa Habari kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu mikakati ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, mafanikio pamoja na changamoto. Sambamba na hilo, Mamlaka imekuwa ikishiriki katika mikutano na warsha mbalimbali kwa lengo la kupanua wigo wa kutoa elimu kwa Taasisi za Umma kama vile *Wiki ya Utumishi wa Umma, Mkutano wa Mwaka wa Maafisa Mawasiliano Serikalini, Mkutano wa Tume ya TEHAMA na Mkutano wa Mwaka wa Wataalam wa Ununuzi na Ugavi n.k*



Baadhi ya wataalamu wa Utafiti na Ubunifu wakisikiliza kwa makini hotuba iliyotolewa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi (Mb) Jijini Dodoma

# Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao

Mamlaka imeendelea kuhimiza uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma. Aidha, Mamlaka imeendelea kutoa Viwango na Miongozo mbalimbali ya Uendeshaji na usimamizi wa matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, ikiwa ni pamoja na kutoa Mafunzo ya uelewa kwa ajili ya utekelezaji wake, ili kuhakikisha kuwa Taasisi hizo zinakuwa na utekelezaji wa Serikali Mtandao wenye tija katika kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa Umma.

Sambamba na hayo, Mamlaka imeendelea kufanya Ukaguzi wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu ya matumizi sahihi na salama ya TEHAMA Serikalini ili kujiridhisha juu ya Ufanisi na Usalama wa Mifumo na Miundombinu hiyo.

Aidha, ili kuhakikisha uratibu wa matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma unazingatiwa ipasavyo kwa mujibu wa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, suala la uongozi na usimamizi wa TEHAMA limekuwa likifanyiwa kazi kwa kuhakikisha kunakuwa na; -

1. Kamati ya Kitaifa ya Uongozi ya Serikali Mtandao - *"National e-Government Steering Committee"*, ambayo Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu Kiongozi;
2. Kamati ya Ufundi ya Serikali Mtandao - *"e-Government Technical Committee"* ambayo Mwenyekiti wake atateuliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Katibu atateuliwa na Mamlaka;
3. Kamati ya Kitaasisi ya Uongozi ya TEHAMA - *"Institutional ICT Steering Committee"*, ambayo Mwenyekiti wake ni Afisa Masuuli wa Taasisi husika na Katibu wake ni Mkuu wa Idara au Kitengo cha TEHAMA; na
4. Uanzishwaji wa Kitengo cha Usimamizi wa TEHAMA (ICT Management Unit) ndani ya Taasisi ya Umma ambayo Mkuu wa Idara ama Kitengo hicho atatoa taarifa moja kwa moja kwa Afisa Masuuli wa Taasisi husika

# Mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini

# Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini

Kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma, Mamlaka imefanikiwa kusanifu, kujenga na kusimamia Mifumo na Miundombinu mbalimbali ya TEHAMA katika taasisi hizo, kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wao na utoaji wa huduma kwa umma, kufanya zipatikane kwa haraka, urahisi na gharama nafuu.


Katika jitihada za kupunguza urudufu wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini, Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara zinazosimamia sekta husika imejenga Mifumo ya kisekta ili kupunguza uhitaji wa kila Taasisi ya Umma kuwa na Mfumo wake, hususan kwa Taasisi ambazo shughuli zake zinafanana.

- **Usanifu na Utengenezaji wa Tovuti za Serikali**

Mamlaka imesanifu na kutengeneza Tovuti mbalimbali za taasisi za umma, ikiwemo Tovuti Kuu ya Serikali na Tovuti Kuu ya Ajira.


i. **Tovuti Kuu ya Serikali**

Mamlaka imesanifu na kutengeneza Tovuti Kuu ya Serikali inayopatikana kupitia kiungo www.tanzania.go.tz, ikiwa na lengo la kutoa taarifa za huduma mbalimbali kwa wananchi kwa urahisi, haraka na wakati wowote. Tovuti hii imeendelea kuboreshwa kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Idara ya Habari - MAELEZO ili kukidhi mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na mahitaji ya Umma ya kupata huduma mtandao.




ii. **Tovuti Rasmi ya Rais**

Mamlaka imebuni, kusanifu na kutengeneza dirisha moja katika Tovuti Rasmi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayopatikana kupitia kiungo www.ikulu.go.tz kwa ajili ya kurusha matangazo mbashara (Live streaming) wakati wowote Rais anapokuwa katika matukio ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Tovuti hii imeunganishwa na Tovuti Kuu ya Serikali (Government Portal) inayopatikana kupitia kiungo www.tanzania.go.tz ambayo hupokea matangazo moja kwa moja wakati yanaporuhusiwa kuruka kupitia tovuti ya Rais




iii. **Tovuti Kuu ya Ajira**

Tovuti Kuu ya Ajira inapatikana kupitia kiungo www.portal.ajira.go.tz, na inasimamiwa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira ikiwa na lengo la kurahisisha mchakato wa ajira Serikalini kwa kupunguza gharama, muda na kuongeza uwazi katika taratibu za uombaji kazi na taarifa za usaili. Tovuti hii ni dirisha kuu la kutangaza nafasi za kazi Serikalini..

### iv. Tovuti za Taasisi za Umma

Mamlaka imeendelea kutoa ushauri na msaada wa kiufundi kwa Taasisi za Umma katika eneo la usanifu, ujenzi, uendeshaji na uwekaji wa taarifa kwenye tovuti zao, ambazo zinarahisisha utoaji na upatikanaji wa taarifa na huduma kwa umma.




### v. Tovuti za Mikoa na Halmashauri

Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imewezesha Mikoa na Halmashauri zote kuwa na Tovuti rasmi ambazo zinatoa taarifa muhimu kwa umma, zilizotengenezwa kupitia Mfumo wa Pamoja wa Kutengeneza Tovuti (Government Website Framework). Hafla ya uzinduzi wa Tovuti hizi ilifanyika tarehe 27 Machi, 2017 Jijini Dodoma. Kuwepo kwa tovuti hizi kunarahisisha mawasiliano na upatikanji wa taarifa kwa umma.





# Mifumo ya Serikali Mtandao

Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Umma, imesanifu, kutengeneza na kusimamia Mifumo Shirikishi na ya Kisekta inayotumiwa na Taasisi za Umma katika utekelezaji wa shughuli za kila siku. Baadhi ya Mifumo hiyo ni pamoja na;

### (i) Mfumo wa Baruapepe Serikalini (eBarua/GMS)

Mfumo huu unaziwezesha Taasisi za Umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa usalama, uharaka na kwa gharama nafuu. Vilevile, Mfumo huu umeimarisha Mawasiliano kwa njia ya baruapepe kwa Taasisi za Umma na kuongeza usalama wa ubadilishanaji taarifa na una kinga dhidi ya wadukuzi hivyo ni salama zaidi kwa usiri wa taarifa za Serikali. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, Taasisi za Umma **702** zinautumia Mfumo huu.



### (ii) Mfumo wa Ofisi Mtandao

Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) umejengwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka Serikalini. Mfumo huu umetengenezwa kwa lengo la kupunguza gharama na kurahisisha mawasiliano, kurahisisha mzunguko wa nyaraka na majalada ndani ya Taasisi za Umma, kurahisisha kufanya uamuzi sahihi na kwa wakati pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, Taasisi za Umma **186** zinatumia Mfumo huu.




### (iii) Mfumo wa Utoaji Huduma za Serikali kwa Simu za Mkononi (MGov)

Kasi ya utoaji wa huduma kwa njia ya simu za mkononi Serikalini ilikua inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uhitaji wa wataalam wa tekinolojia husika ambao ni wachache Serikalini, uhitaji wa mikataba ya kibishara baina ya taasisi ya umma na makampuni ya simu, ambayo taratibu zake zinachukua muda mrefu, gharama ya kutangaza huduma husika ili ifahamike na wananchi wengi pamoja na gharama ya tekinolojia husika, ambapo taasisi nyingi hushindwa kumudu hivyo kupelekea kuacha kutoa huduma kwa njia hii.

Ili kutatua changamoto hizo, Mwaka 2015, Wakala ilijenga Mfumo jumuishi wa utoaji wa huduma kwa njia ya simu za mkononi Serikalini (MGOV) ambao umeendelea kuboreshwa kutegemeana na mahitaji. Mfumo wa MGov umerahisisha utoaji wa huduma kwa njia ya simu za mkononi ambayo ni bora na ya haraka.


Mfumo wa mGOV umeunganishwa na watoa huduma wote wa simu za mikononi nchini Tanzania ambao ni TTCL, Airtel, Vodacom, Tigo/Zantel na Halotel unatoa huduma za ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) kupitia namba jumuishi **15200** na **15201** pamoja na huduma za menyu ya **USSD** kupitia namba jumuishi ***152*00#**. Vilevile, Mfumo wa **MGOV** unaruhusu taasisi za umma kutoa huduma kupitia namba binafsi za taasisi, mfano wa namba binafsi za taasisi ni ***199#** ya Wizara ya Afya inayotoa huduma na taarifa za **COVID-19** na ***113#** ya **PCCB** inayotoa huduma ya kuripoti matukio ya rushwa.

Hadi kufikia Julai, 2022 taasisi zaidi ya 254 zilikuwa zineunganishwa na kuutumia Mfumo wa mGOV kutoa huduma. Baadhi ya huduma hizo ni SMS za ununuzi wa umeme (LUKU), SMS za huduma za malipo ya Serikali (GePG), Huduma za kikodi (TRA), Huduma za Ardhi, Huduma za afya (NHIF, CHF n.k), Huduma za Kilimo, Ajira, Maji, Elimu, Sheria, Haki, n.k. Zaidi ya miamala 500 milioni ya jumbe fupi za maandishi pamoja na ya USSD inashughulikiwa na mfumo wa mGOV kwa mwaka.ghulikiwa na mfumo wa mGOV kwa mwaka.kwa mwaka.



### iv) Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB)

Mamlaka imesanifu, kutengeneza na kuusimamia Mfumo unaowezesha Mifumo mbalimbali ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa unaojulikana kama Government Enterprise Service Bus- GovESB. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, Mifumo **26** ya Taasisi **23** imekuwa ikibadilishana taarifa kupitia Mfumo huu




### (v) Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS)

Mfumo huu unatumika kusimamia Rasilimali pamoja na shughuli za kila siku za kiutendaji ndani ya Taasisi, kuboresha utendaji kazi na kupunguza gharama za uendeshaji. Mfumo huu una Moduli 20 zinazowasiliana na kubadilishana taarifa. Moduli hizo ni pamoja na: Mipango, Bajeti, Uhasibu, Usimamizi wa Wateja, Ununuzi, Usimamizi wa Huduma, Usimamizi wa Vyombo vya Usafiri, Rasilimali watu, Likizo, Ankara, Ripoti n.k. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, jumla ya Taasisi za Umma 33 zinatumia mfumo huu. Pamoja na shughuli za kila siku zinazofanywa na ERMS, Taasisi 10 zimefanikiwa kuandaa hesabu za fedha kupitia mfumo huu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.




### (vi) Mfumo wa e- Mikutano

Mfumo huu umesanifiwa na kutengenezwa ili kuziwezesha Taasisi za Umma kufanya vikao na mikutano kwa njia ya mtandao bila washiriki kulazimika kukutana ana kwa ana. Mfumo huu umetengenezwa kwa kuzingatia usalama wa taarifa. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, Taasisi za Umma 156 zilikuwa zimeunganishwa na kutumia Mfumo huu.




### (vii) Mfumo wa Vibali vya Safari za Watumishi Nje ya Nchi (e-Vibali)

Mfumo huu umesanifiwa na kutengenezwa kwa manufaa ya Serikali ili kusimamia na kuratibu utoaji wa Vibali vya kusafiri nje ya Nchi kwa watumishi wa Umma. Mfumo huu unapatikana kupitia **https://safari.gov.go.tz.** Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, jumla ya Taasisi za Umma **619** zinatumia Mfumo huu.


### (viii) Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini (Government ICT Services Portal-GISP)

Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini (GISP) inayopatikana kupitia kiungo https://gisp.gov.go.tz, ni dirisha moja la huduma za TEHAMA Serikalini linalohusika na utoaji ithibati za Miradi mbalimbali ya TEHAMA ya Taasisi za Umma pamoja na utoaji msaada wa kiufundi. Tovuti hii inahakikisha usimamizi bora wa Miradi ya TEHAMA, utoaji wa huduma bora na ushirikishwaji wa Taasisi za Umma kwa ufanisi. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, Taasisi za Umma **546** zimewasilisha Miradi ya TEHAMA kupitia Tovuti hii.





### (ix) Mfumo wa Huduma kwa Wateja (Help Desk)

Mfumo huu umesanifiwa na kutengenezwa ili kutoa huduma na msaada wa kiufundi kwa Taasisi za Umma zinazotumia huduma zitolewazo na Mamlaka. Mfumo huu unapatikana kupitia kiungo https://helpdesk.gov.go.tz, na mteja anaweza pia kupiga simu ya Mkononi kupitia namba 0764 292 299 au 0763 292 299 au kwa kutuma baruapepe egov.helpdesk@ega.go.tz. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, jumla ya Taasisi za Umma **613** zinautumia Mfumo huu.




### (x) Mfumo wa Kusimamia Mafunzo na Semina (TSMS)


Mfumo huu umetengenezwa na Mamlaka kwa ajili ya utunzaji kumbukumbu na taarifa mbalimbali zinazohusu mafunzo, semina, warsha na mikutano mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikatano ya mwaka ya Serikali Mtandao. Mfumo huu unapatikana kupitia anuani **https://tsms.ega.go.tz**, hadi kufikia Mwezi Julai, 2022 jumla ya Taasisi **586** zilikuwa zimeunganishwa na kuutumia Mfumo huu.



### (xi) Mfumo wa Kielektroni wa kutuma, kupokea, na kufuatilia Malalamiko, mapendekezo, Maulizo na Pongezi (eMrejesho)

Mfumo huu umesanifiwa na kujengwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kama sehemu au njia ya wananchi kuifikia Serikali yao. Mfumo huu umetengenezwa kwa lengo la kumsaidia mwananchi kupunguza gharama na kuokoa muda wa kutembea umbali mrefu ili kuwasilisha maoni, mapendekezo au kufuatilia malalamiko yake.

Aidha, Mfumo huu umesaidia kuongeza ufanisi wa Taasisi za Umma katika utoaji wa huduma kwa wakati na kwa ubora kwa kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi. Mfumo huu unapatikana kupitia kiungo **https://emrejesho.gov.go.tz** au kwa kupakua program inayopatikana kwenye simu janja au kupitia msimbo ***152*00#**. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, Taasisi za Umma **363** zinautumia Mfumo huu.





# Mifumo ya Kisekta

Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Umma imetengeneza Mifumo mbalimbali ya kisekta ambayo imeleta mapinduzi makubwa katika uendeshaji wa Serikali hususani katika udhibiti wa makusanyo pamoja na kurahisisha na kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali. Mifumo hiyo ni kama vile;

### (i) Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG)

Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imesanifu na kutengeneza Mfumo shirikishi wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG) ili kuboresha uwazi na udhibiti katika ukusanyaji mapato ya Serikali.

Hadi kufikia Mwezi Juni, 2022, jumla ya Taasisi za Umma **766** zinazotoa huduma za malipo zilikuwa zimeunganishwa katika Mfumo huu, zikiwemo taasisi za Fedha (Benki) **28** na Kampuni **7** za Simu zinazotoa huduma za kifedha kupitia simu za mkononi.




### (ii) Mfumo wa Pamoja wa Utoaji Ankara kwa Mamlaka za Maji Nchini (MAJIIS)

Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya maji, imesanifu na kutengeneza Mfumo wa MAJIIS kwa lengo la kurahisisha uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Mamlaka za maji na Bodi za maji za Mabonde nchini Tanzania. Taasisi nyingi za maji hazikuwa na Mifumo inayorahisisha utendaji kazi na baadhi ya taasisi zilikuwa na Mifumo ambayo ufanisi wake haukuwa wa kiwango cha kuridhisha hivyo kupelekea mamlaka hizo kupata changamoto ya utoaji wa huduma bora, ugumu wa upatikanaji wa taarifa za kiutendaji pamoja na za makusanyo kuchukua muda mrefu na wakati mwingine taarifa hizo kutokuwa sahihi.

Mfumo wa MAJIIS umerahisisha utoaji huduma na ukusanyaji mapato, umeongeza ufanisi, uwazi, na umesaidia kupunguza mianya ya rushwa kwa kuondoa ulazima wa mteja na mtoa huduma (taasisi ya maji) kukutana ana kwa ana ili kupata huduma. Kupitia Mfumo huu mteja anaweza kujihudumia mwenyewe kupitia simu yake ya mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** kisha atachagua namba **6** - Maji, kisha namba - **1** Huduma za pamoja za maji ambapo atakutana na orodha inayoonesha huduma mbalimbali za maji na atachagua kadiri ya hitaji lake.

Mfumo wa MAJIIS unafanya tathmini ya matumizi ya maji ya mteja katika vipindi tofauti vya matumizi ili kuhakikisha ankara anayopatiwa mteja ni sahihi kutokana na matumizi yake. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022 jumla ya Mamlaka za maji pamoja na Bodi za maji za mabonde 82 kati ya 94 zilizopo, zilikuwa zimeunganishwa na kutumia Mfumo wa MAJIIS. Mfumo wa MAJIIS unatumiwa pia na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).






### iii) Mfumo wa Pamoja wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha (TeSWS)

Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na Taasisi mbalimbali za udhibiti wa shughuli za forodha (Other Government Departments – OGDs), imesanifu na kutengeneza Mfumo huu ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuongeza uwezo wa nchi kukabiliana na ushindani wa kibiashara kimataifa, kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kurahisisha uondoshaji Shehena maeneo ya Forodha. Maeneo hayo ya Forodha ni pamoja na Bandari, Viwanja vya Ndege, Maghala ya Forodha, Posta na maeneo ya mipakani.

Hadi kufikia Mwezi Septemba, **2022** Mfumo huu umekuwa ukitumika na Kampuni za Wakala **877** kati ya Kampuni za Wakala **1,142**. Aidha, Mfumo huu umepokea na kuchakata kadhia (customs declarations) **459,671,** kati ya hizo zilizokamilika na kuwezesha shehena kulipiwa kodi na kutoka bandarini na maeneo mengine ya forodha ni **438,126** na kadhia zilizosalia zipo kwenye Taasisi wadau katika ugomboaji. Kwa sasa, Mfumo huu unapokea na kuchakata wastani wa kadhia **1,200** kwa siku ukiondoa siku za Jumamosi, Jumapili na sikukuu. Aidha, Mfumo huu unatumiwa na kampuni za watunza shehena **"Cargo Keepers"** zipatazo 218. Vilevile, Mfumo wa TeSWS unawezesha Taasisi wadau kufanya ukaguzi wa pamoja wa shehena (joint inspection).

Mfumo wa TeSWS umeunganishwa na unabadilishana taarifa na Mfumo wa Kuondosha Shehena Katika Maeneo ya Forodha (TANCIS) wa TRA pamoja na Mifumo ya Taasisi za Udhibiti ikiwemo Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC). Mfumo huu unapatikana kupitia **https://tesws.gov.go.tz/login**




### (iv) Mfumo wa kusimamia Rasilimali Watu Serikalini (HCMIS)


Mamlaka kwa kushiriana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imesanifu na kutengeneza Mfumo huu unaotumika kusimamia rasilimaliwatu katika utumishi wa umma, kukusanya, kutunza na kuwasilisha taarifa mbalimbali za watumishi wa Umma kuhusu masuala ya kiutumishi pamoja na kukokotoa mishahara ya kila mwezi ya watumishi.

### (v) Mfumo wa Tiketi za Kieletroni (e -Ticketing and Cargo System)

Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania imesanifu na kutengeneza Mfumo huu ambao ni mahsusi kwa ajili ya ukataji wa tiketi kieletroni au uhifadhi wa siti (Booking). Mfumo huu unasaidia kupunguza upotevu wa mapato na gharama za uchapishaji wa tiketi, ikiwa na lengo la kumsaidia mteja kukata tiketi bila kufika katika ofisi inayohusika.

### (vi) Bunge Mtandao (e-Parliament)


Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge imesanifu na kutengeneza Mfumo wa Bunge Mtandao ambao hutumika kuhifadhi taarifa za Bunge kama vile Miswada na Sheria, Hotuba, Kumbukumbu za vikao vinavyofanyika katika vipindi vya Bunge, Kanzidata ya waheshimiwa wabunge na majimbo wanayowakilisha. Mfumo huu unasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mfumo huu umeungana na Moduli inayoendesha shughuli za Bunge kielektroniki.



### (vii) Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU)

Mamlaka kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imesanifu na kutengeneza Mfumo huu unaolenga kurahisisha Ukaguzi, Usimamizi, na Uendeshaji wa vyama vya ushirika ili kuongeza Ufanisi, Uwazi na Uwajibikaji utakaoboresha utendaji na kuchochea mabadiliko ya Kiuchumi kwa kurahisisha huduma na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Aidha, Mfumo huu unasaidia kupata taarifa kutoka kwenye vyama na kutoka kwa wadau mbalimbali wa Ushirika kwa wakati na usahihi. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, jumla ya **Mikoa minne (4)** ilikuwa imesajiliwa. Aidha, jumla ya vyama **534** ambavyo ni **AMCOS** na **SACCOS** vya mikoa hiyo vyenye wanachama zaidi ya **19,521** vimesajiliwa




### (viii) Mfumo wa Uendeshaji Shughuli za Wakala wa Ununuzi Serikalini (GIMIS)

Mamlaka kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), imesanifu na kutengeneza Mfumo wa GIMIS kwa lengo la kurahisisha uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Wakala. Mfumo huu unawezesha taasisi nunuzi kupata huduma za ununuzi wa vifaa, mafuta na magari kutoka kwa wakala pamoja na huduma ya ugomboaji na uondoshaji wa mizigo.

Aidha, Mfumo huu unaratibu mchakato mzima wa ununuzi wa magari ya Serikali kuanzia uombaji wa kibali, utoaji wa "specification", ununuzi hadi usajili wa gari. Ambapo taasisi zinazohusika katika mchakato huu zikiwemo Wizara ya Ujenzi, Ofisi ya Waziri Mkuu, GPSA, TEMESA na Wizara ya Fedha hufanya kazi katika mfumo mmoja hivyo kurahisisha ufuatiliaji na kuongeza ufanisi katika utendaji.

Pia, Mfumo huu unasaidia taasisi nunuzi kupata taarifa za manunuzi ya vifaa na mafuta yaliyofanyika katika taasisi zao kwa urahisi, usahihi na kwa wakati pindi zinapohitajika. Hadi kufikia Mwezi Januari, 2023, jumla ya taasisi nunuzi **(5,730)** zilikuwa zimesajiliwa na kupata huduma mbalimbali kupitia mfumo huu.

Mfumo huu unapatikana kupitia: **https://gimis.gpsa.go.tz**



# Miundombinu Shirikishi ya TEHAMA

Miundombinu bora na shirikishi ya TEHAMA ni muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma kwa umma. Kwa kuzingatia umuhimu wa usalama wa Mifumo ya TEHAMA, Serikali inaweka miundombinu ya TEHAMA ambayo inaziwezesha Taasisi za Umma kushirikiana katika matumizi ya rasilimali za TEHAMA ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano. Miundombinu iliyopo ni pamoja na Mtandao wa Serikali (GovNet), Vituo vya Kitaifa vya Data na Masafa ya intaneti.



(i) **Mtandao wa Serikali (GovNet)**

Mtandao wa Mawasiliano Serikalini ni sehemu ya Miundombinu ya TEHAMA ya Serikali unaosimamiwa na kuratibiwa na Mamlaka kwa niaba ya Serikali. Mtandao huu umewezesha kuunganishwa kwa Taasisi za serikali (MDAs na LGAs) kupitia Mkongo wa Taifa. Lengo kuu ni kuhakikisha usalama wa data na taarifa katika taasisi za umma zilizopo katika mifumo yao, pamoja na kupunguza gharama za mawasiliano ya intaneti kwa Taasisi zote zilizounganishwa. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022, jumla ya Taasisi za Umma 330 zilikuwa zimeunganishwa.

Vilevile, Mamlaka inaendelea kutoa msaada wa kiufundi na kuzijengea uwezo taasisi za umma kusimamia na kuendesha miundombinu ya mawasiliano ya ndani (LAN) na mawasiliano kwa ya simu (VoIP)



(ii) **Kituo cha Kuhifadhia Data na Mifumo ya Serikali**

Mamlaka imeendelea kutoa huduma za uhifadhi wa Mifumo kwa Taasisi za Umma, kuhakikisha usalama na uhakika wa upatikanaji wa mifumo hiyo. Aidha, Mamlaka inaendelea kuboresha na kusimamia uendeshaji wa vituo vya Kuhifadhi data pamoja na Miundombinu ya Mifumo Shirikishi ili viweze kuhifadhi mifumo mingi zaidi kwa kutumia Teknolojia za kisasa. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2022 jumla ya Taasisi za Umma 124 zimehifadhi Mifumo yao katika Vituo hivyo.

(iii) **Masafa ya intaneti (Internet Bandwidth)**

Serikali kupitia Programu ya Kikanda ya Miundombinu ya Mawasiliano **(Regioanl Communication Infrastructure Programe – RCIP)** iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia, ilinunua haki miliki ya kutumia (Indefeasible Right of Use - IRU) masafa ya intaneti yenye kasi ya 1.55 Gbps kwa muda wa miaka 10 ambapo Taasisi za Umma **490** zinanufaika.


Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni kama vile Wizara, Idara, Wakala, Hospitali, Shule na Taasisi za Elimu ya Juu. Upatikanaji wa masafa haya unasaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Haki miliki hii imeongezewa muda wa Miezi sita (6) toka ilipofikia ukomo Mwezi Juni, 2022 na masafa yakiongezwa kufikia kasi ya 5 Gbps. Aidha, Serikali kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijiti (DTP), inalenga kununua haki miliki kwa kipindi kisicho pungua Miaka 10 kwa masafa yasiyo pungua kasi ya 20 Gbps kutokana na ukuaji wa matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma kwa wananchi. Taratibu za ununuzi zinaendelea.

# Tafiti na bunifu za maendeleo ya Serikali Mtandao

Mwaka 2019, Mamlaka ilianzisha Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Maendeleo ya Serikali Mtandao kwa lengo la kuratibu tafiti na bunifu za maendeleo ya jitihada za Serikali mtandao ili kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa Umma, pamoja na kujengea uwezo na kukuza vipaji vya vijana wa kitanzania katika eneo la serikali mtandao.

Mamlaka inashirikiana Taassisi na Vyuo Vikuu 14 kwa ajili ya kutambua vipaji na bunifu mbalimbali kutoka kwa vijana wanaosoma au waliomaliza katika Vyuo Vikuu hivyo, ambapo hadi mwishoni mwa mwezi Septemba, 2022 Jumla ya wanafunzi 201 wameshiriki katika shughuli za kitafiti zilizoibua bunifu mbalimbali.

Kituo hiki kinatoa mazingira wezeshi kwa wanafunzi na watafiti mbalimbali kufanya tafiti zao katika maeneo wanayopenda, ikiwemo katika Teknolojia zinazochipukia, kama vile *Block Chain, Internet of Things n.k.*





Mfumo wa eMrejesho unaowezesha kutuma,kupokea na kufuatilia Malalamiko, Mapendekezo, Maulizo na Pongezi ikiwa ni zao la kituo cha Utafiti na Ubunifu

# Mafunzo ya Serikali Mtandao

Kupitia Kituo cha Utafiti na Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao (e-GovRDIC), Mamlaka imekuwa ikiratibu utoaji wa mafunzo kwa Watumishi wa Umma kwa kushirikiana na Taasisi za Elimu ya Juu ili kuwajengea uwezo watumishi hao kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao.

Aidha, Taasisi hizo za Elimu ya Juu zinatoa mafunzo hayo kwa makubaliano maalumu na Mamlaka baada ya kupewa mafunzo kama wakufunzi katika maeneo ya huduma mpya za serikali mtandao. Lengo la Mamlaka ni kupanua wigo wake kuzifikia Taasisi za Umma kwa haraka..



# Ushirikiano na wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar

Katika kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wa serikali mtandao, Mamlaka imefanikiwa kuanzisha na kuendeleza ushirikiano na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar kupitia Hati Rasmi ya Ushirikiano (MoU) katika utoaji wa mafunzo na huduma kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao Zanzibar. Kupitia ushirikiano huu, yametolewa mafunzo mbalimbali katika eneo la usalama wa serikali matandao na usimamizi na viwango vya serikali mtandao.

Aidha, mifumo kadhaa imefanyiwa marekebisho ili iweze kutumiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), na sasa tayari inatumika. Mifumo hii pamoja na: Mfumo wa Barua Pepe Serikalini, Mfumo wa Masjala, Mfumo wa Malipo Zanzibar (ZanMalipo), Mfumo wa Ajira (ZanAjira), e-Wawakilishi, Mfumo wa Ankara za Maji (MAJIIS) kwa ajili ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Pia, Mamlaka inashirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar katika utoaji wa huduma ya miundombinu ya serikali mtandao.



# SERIKALI MTANDAO MIAKA 10 IJAYO

# Serikali Mtandao Miaka 10 ijayo

## • Mwelekeo

Katika kipindi cha miaka 10 ijayo, Mamlaka itaandaa na kutekeleza mikakati madhubuti ili serikali mtandao ifikie kuwa:

1. Sehemu moja ambayo huduma mtandao zote zitakuwa zinapatikana.
2. Uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka, hasa zile za akili bandia, sarafu za kidijiti na teknolojia za kifedha, ili kuwezesha maboresho ya kiutendaji katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma.
3. Kuwa na vijana wa kitanzania wenye uwezo mkubwa wa ubunifu katika utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao.
4. Uzalishaji wa vifaa na miundombinu ya TEHAMA (Hardware) ndani ya Tanzania
5. Mifumo na miundombinu ya serikali mtandao iliyo bora na imara zaidi.
6. Ubadilishanaji kamili wa taarifa miongoni mwa mifumo tumizi ya kitaasisi na kisekta ya serikali mtandao.
7. Uwezo mkubwa wa kudhibiti matishio ya usalama mtandaoni
8. Kuwa na namba moja ya utambuzi kurahisisha utoaji wa huduma mtandao kwa umma.

## • Maeneo ya Kipaumbele

Ili kufikia serikali mtandao inayotakiwa katika kipindi kijacho, kipaumbele cha miaka miwili ya awali, Mamlaka kitakuwa katika maeneo yafuatayo:

i. Kuendelea kupitia na kutathmini hali ya usalama wa Mifumo na Miundombinu ya Serikali Mtandao na kuzishauri Taasisi za Umma katika maeneo ya kuboresha, pamoja na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA inafanya kazi wakati wote kwa ufanisi na usalama;

ii. Kuendelea kuunganisha Mifumo ya Taasisi za Umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kubadilishana Taarifa (Government Enterprise Service Bus - GovESB).

iii. Kuendeleza shughuli za tafiti na ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa umma na kuwezesha matumizi sahihi ya teknolojia mpya zinazoibuka;

iv. Kupanua uwezo wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network) na kuufikisha katika Wilaya zote nchini ili kurahisisha utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao kwa taasisi za umma nyingi zaidi, ikiwemo kutumia mifumo shirikishi ya serikali mtandaom, kama mifumo ya barua pepe, masjala na e-vibali.

v. Kuendelea kupitia na kukagua Mifumo ya kimkakati, kisekta na kitaasisi ili kuhakikisha kuwa imetengenezwa na inatumika kwa kufuata Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo iliyopo na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake; na

vi. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi katika kusimamia Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, pamoja na kutoa mafunzo kwa watumiaji kuhusu matumizi sahihi na salama ya Mifumo na Miundombinu ya Serikali Mtandao.

vii. Kuendelea kujenga uwezo wa Mamlaka wa kusimamia utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma na uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao iliyoidhinishwa.matumizi sahihi na salama ya Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA.

# Matukio mbalimbali



Picha ya pamoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista mhagama na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao baada ya kuizindua bodi hiyo Novemba 2, 2022.



Aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (Katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na aliyekua Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao Dkt. Jabiri Bakari na viongozi wengine wakati wa Kikao kazi cha pili cha Serikali Mtandao kilichofanyika Februari 2019 Jijini Dodoma



Washiriki mbalimbali wa Kikao kazi cha Serikali Mtandao wakisikiliza kwa makini mada zilizotolewa wakati wa kikao hicho kilichofanyika Februari 2019 Jijini Dodoma



Wakuu wa Idara na vitengo vya TEHAMA Serikalini wakisikiliza kwa makini wasilisho lililotolewa wakati wa kikao kazi cha wakuu wa Idara za TEHAMA ili kuwajengea uwezo katika kusimamia Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019.



Aliyekuwa Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbasi akisaini katika kitabu cha wageni alipotembelea Makao Makuu ya Wakala yaliyopo Mji wa Serikali Dodoma Agosti 28, 2019




Aliyekuwa Mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Serikali mtandao Dkt. Jabiri Bakari akiwa na Tuzo aliyokabidhiwa na Tume ya TEHEMA kwa kuthamini mchango wake katika kuitekeleza kwa vitendo azma ya Serikali kuwa ya Kidijitali.



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ***Mhe. Kundo A. Mathew (Mb)*** akimkabidhi tuzo ya Udhamini Mkurugenzi wa Miundombinu na Uwezeshaji wa Mamlaka ***Bw. Benjamin Dotto*** kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka Septemba 23, 2022 katika viwanja vya ndaki ya TEHAMA Kijitonyama jijini Dar Es Salaam.




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ***Mhe. Kassim Majaliwa*** akimkabidhi cheti cha udhamini wa KongamanoMkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA ***Bw. Ricco Boma*** wakati wa Kongamano la Sita (6) la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lililofanyika tarehe 19 Septemba 2022 jijini Dodoma.

ega_tanzania ega online tv

# Michezo












**Mamlaka ya Serikali Mtandao,**
**S.L.P 2833,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Mtandao.**
**DODOMA**

Barua Pepe: info@ega.go.tz
Tovuti: www.ega.go.tz

"Karibu tuijenge Serikali Kidijitali"

ega_tanzania